

## Maswali

1. Ni siku ngapi Musa alikuwa mlima wa Sinai?
2. Watu wa Israeli walitaka Haruni afanye nini?
3. Hao watu walimpa Haruni nini?
4. Haruni alifanyia nini dhahabu?
5. Mungu alimwambia Musa nini huko mlimani?
6. Kutoka mlimani Musa alibeba nini?
7. Musa alisikia nini aliposhuka chini?
8. Musa alifanyaje hiyo ndama ya dhahabu?
9. Nani walikuwa upande wa Bwana?
10. Watu wangapi walikufa?

## Majibu

1. Musa alikuwa mlimani siku 40
2. Walitaka Haruni awafanyie miungu wapya
3. Hao watu walimpa Haruni pete za masikio za dhahabu.
4. Haruni alitengeneza ndama ya dhahabu.
5. Mungu alimwambia Musa kwamba watu walikuwa wamefanya ndama ya dhahabu.
6. Musa alibeba mbao 2 za mawe – amri 10
7. Musa alisikia nyimbo.
8. Musa alichoma hiyo ndama akaisaga na kumwaga ndani ya maji ya kunywa.
9. Makuhani walikuwa upande wa Bwana.
10. Watu elfu tatu walikufa.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

# 18 Ndama ya Dhahabu

## Marejeo

Kutoka 24 + 32

## Kiini cha somo

Kuonyesha utakatifu wa Mungu na ni yeye tu anastahili kuabudiwa.

## Maneno maalum

1. Safari + Sinai + mlima + Mungu apeana sheria + utukufu wa Mungu + siku 40 + Musa apotea?
2. Tutengeneze miungu wapya + Haruni + pete za masikio + ndama ya dhahabu
3. Karamu + kucheza na kuimba + Mungu anakasirika + Musa anamsihi Mungu
4. Musa anatoka mlimani + kasirika + avunja mbao za mawe + watu waovu wauawa

**18.1** Walipovuka Bahari ya Shamu Musa na wana wa Israeli walisafiri jangwani. Walifika mlima wa Sinai. Mungu alimwambia Musa akwee (panda) mlimani ili ampe sheria zenye lazima wana wa Israeli watii. Tunaziita hizi sheria (amri 10). Musa alikwea juu ya mlima na kuona utukufu wa Mungu. Ulikuwa kama moto juu ya huo mlima.


Musa alikuwa mlimani kwa siku 40. Watu hao Waisraeli walifikiri Musa hatarudi kutoka mlimani. Walienda kuona Haruni.

**18.2** “Tutengenezee Miungu wapya,” walimwambia. “Hatujui yaliyompata Musa.”

Haruni alisema, “Toa hizo pete za dhahabu zilizovaliwa kwa masikio ya wake na binti wenu, mniletee.”

Walitoa pete za dhahabu kutoka masikioni na kumpa Haruni. Akatengeneza ndama ya dhahabu.

Wakasema, “Huyu ndiye Mungu aliyetutoa Misri.” Haruni alipoona ndama ya dhahabu, akajenga madhabahu mbale yake.



**18.3** “Kesho tutafanya karamu ya kumwabudu Bwana,” Haruni aliwaambia hao watu. Siku ufuatayo watu waliamka mapema. Wana wa Israeli wakasimama mbele ya ndama na kumtolea dhabihu. Wakakaa sitarehe na kuwa na karamu. Waliimba na kucheza wakizunguka hiyo ndama ya dhahabu. Mungu aliona yote waliyofanya wakati Musa hakuwepo. Mungu alimwambia Musa, “Wana wa Israeli wametengeneza ndama ya dhahabu na wanaiabudu.”

Mungu aliwaka kwa hasira. “Nitawaaribu,” Mungu alimwambia Musa. Musa alimsihi Mungu, “Kama hautawasamehe basi niharibu mimi.” “Nitawaaribu waliofanya dhambi,” Mungu alisema.

**18.4** Musa aliteremka kutoka mlimani, mkononi mwake amebeba mbao mbili kubwa ambapo Mungu aliandikia Waisraeli sheria. Musa alisikia watu wanaimba na kufanya kelele. Akaona ndama ya dhahabu, akakasirika na kutuba hizo mbao chini. Hizo mbao zilivunjika. “Mbona mmefanya hii dhambi kubwa?” aliuliza Haruni.



Musa alichukua hiyo ndama na kuchoma kwa moto. Akaisaga na kutupa ndani ya maji. Aliuliza kila mtu kukunywa hayo maji. “Nani ako upande wa Mungu? Nani anataka kuabudu Mungu?” Musa aliuliza, “kuja kwangu.”

Makuhani wote walienda upande wa Musa. Aliwaambia washike panga wawauwe hao watu waovu waliomwabudu ndama. Makuhani walifanya vile Musa alisema na kawauwa watu elfu tatu.

Tunajifunza somo kubwa, ya kwamba tusiabudu kitu chochote ila Bwana Mungu. Lazima tumpende na kumtii Mungu peke yake.